KISWAHILI KARATASI 1

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 - 7.

Mataifa ya Afrika yanajivunia mila na desturi ambazo zimewawezesha watu wa nchi hizi kuishi kwa umoja na amani. Hata hivyo, hakuna jambo lolote jema lisilo na ila. Baadhi ya mila ni potovu na zisizokubalika katika dunia ya sasa.

Kati ya mila zilizopitwa na wakati ni ile ya ukeketaji wa wasichana. Waafrika walikuwa na sababu za kuwakeketa wasichana lakini kulingana na utafiti uliofanywa, madhara yake ni mengi zaidi, yakiwa ni pamoja na hatari ya kuambukizwa ugonjwa hatari wa ukimwi kwa sababu kisu kimoja huenda kikatumiwa kuwatahiri wasichana wengi. Hata hivyo, tatizo kubwa zaidi ni kuwa, wasichana hawa hunyimwa nafasi ya kuendelea na masomo na badala yake huolewa na watu ambao wao wenyewe hawawapendi. Tunapinga vikali ndoa za lazima. Hili ni janga, ni balaa. Wahusika wanapaswa kusimama imara na kukataa katakata.

Sopiato, msichana mrembo na mwenye akili tambuzi aliamua kukabiliana nalo. Siku ilikuwa imewasili. Siku yao ya kupashwa tohara. Kila kitu kiliandaliwa barabara. Mgeni mheshimiwa aliwasili. Naye hakuwa mwingine bali ni chifu wa kata ya Bondeni. Alivaa ngara maridadi sana. Alibebewa kigoda chake na msaidizi wake. Chifu huyu wa kitamaduni alikuwa na ushawishi mkubwa. Alikuwa na walinzi waliobeba silaha za kila aina.

Sopiato alilia kwa huzuni. Alikumbuka masomo yake akatokwa na machozi. Alionyesha ukarimu wa kutoa machozi. Kilio si dawa. Mambo haya hayakuwashua wazee. Sopiato alikuwa ni kama kifaranga mikononi mwa mwewe na tujujavyo dua ya kuku haimpati mwewe.

1. Ni nini umuhimu wa mila na desturi za kiafrika?
    A. Utengano na amani
    B. Umoja na amani
    C. Ujuzi wa amani
    D. Amani na shukrani
2. Kuna tatizo gani na mila nyingine za kiafrika?
    A. Zinarudisha maendeleo nyuma kwa kuwanyima watu wengine haki za kujiendeleza.
    B. Zinawapa wanafunzi haki za kuendelea na masomo.
    C. Zinawafanya wavulana wengine kukeketwa.
    D. Wasichana wengine husoma sana na kupata kazi nzuri.
3. Ni janga gani linaweza kusababishwa na tohara ya wasichana?
    A. Kuvunjika kwa ndoa.
    B. Ugonjwa wa ukimwi.
    C. Wasichana kutoroka na kupotea.
    D. Wasichana kusoma vizuri na kupata madaraka makubwa.
4. Unafikiri ni tukio gani hufuata baada ya wasichana kupashwa tohara?
    A. Kusoma kwa bidii na kupata kazi.
    B. Kukimbilia kwenye mashirika yasiyo ya kiserikali.
    C. Kutafutiwa wachumba.
    D. Kuolewa kwa hiari na watu wanaowapenda wao wenyewe.
5. Kuna maana gani kusema Chifu alikuwa na ushawishi mkubwa?
    A. Alikuwa akifanya mambo baada ya kushawishiwa kufanya hivyo.
    B. Alikuwa akishawishi katika kuwathiri wasichana.
    C. Maneno yake yalikuwa yakitiliwa maanani na bila shaka aliheshimiwa.
    D. Alibebewa kigoda chake na msaidizi wake.
6. Katika maisha ya chifu, ni jambo gani ambalo tunaona anatilia mkazo zaidi?